## Jinsi ya kuwasilisha malalamishi kwa Tume

Pata Fomu ya Msaada kutoka kwa ofisi za Tume ama kwa Ofisi za Mwana Sheria Mkuu wa Kenya na Idara ya Haki zilizoko kwa Kaunti tofauti tofauti nchini ama kutoka kwa tovuti yetu www.acc.go.ke BILA MALIPO YOYOTE

Jaza Fomu hiyo na uambatanishe hati za kujitambulisha na ushahidi mwengine wowote wa kuimarisha malalamishi yako

Wasilisha fomu hiyo ya msaada ikiwa na sahihi yako kwa ofisi za Tume wewe binafsi, ama kupitia kwa gari za huduma za uchukuzi na mawasiliano ama utume nakala iliyochanganuliwa kwa barua pepe ya Tume ambayo ni: acc@ag.go.ke

## ANWANI YA MAWASILIANO:


Katibu
Tume ya Kupokea Malalamishi Dhidi ya Mawakili
Ofisi ya Mwana Sheria Mkuu na Idara ya Haki
Jumba la Benki ya Co-operative,
Orofa ya Ishirini (20)
Haile Sellassie Avenue, Nairobi
SLP 48048 – 00100, Nairobi
Simu: +254-20-2224029, 2240337
0700 572 929 ama 0732 529 995
Anwani ya Barua Pepe: acc@ag.go.ke
Tovuti: www.acc.go.ke


*Wageni wanaombwa kuripoti
Kwa Dawati la Mapokezi lililopo
Orofa ya Ishirini (20)
Jumba la Benki ya Co-Operative
Haile Sellassie Avenue, Nairobi*

Tunahimiza wananchi na umma kuwasilisha malalamishi yao (bila malipo yoyote) kupitia tovuti yetu ya: www.acc.go.ke

HARAMBEE

### JAMHURI YA KENYA

## OFISI YA MWANA SHERIA MKUU NA IDARA YA HAKI

## *TUME YA KUPOKEA MALALAMISHI DHIDI YA MAWAKILI*

## Maono:

*Kuhamasisha Imani Kuu kwa Umma katika Taaluma ya Kisheria*

# Kurunzi ya Tume


## Kutuhusu

Tume ya Kupokea Malalamishi dhidi ya Mawakili ("Tume") ni idara katika Ofisi ya Mwana Sheria Mkuu wa Kenya na Idara ya Haki. Tume ina majukumu ya kupokea, kuchunguza, kuhimiza upatanisho na kuendesha mashtaka yanayoshirikisha malalamishi dhidi ya mawakili, kampuni za mawakili, mfanyikazi ama mtu yeyote katika kampuni za mawakili.

## Dhamira/Azimio

Tume imejitolea kuhakikisha kuwa imetoa huduma za ufanisi wa hali juu wakati inaposhughulikia malalamishi yanayohusiana na utovu wa nidhamu wa mawakili katika taaluma yao ya kisheria.

## Maadili ya Kimsingi




## Malalamishi yanayoweza kuripotiwa kwa Tume?

**Wakili:**

1. Kushikilia ama kuzuia fedha za mteja.
2. Kukosa kuorodhesha jinsi pesa za mteja zilitumika.
3. Kutomfahamisha mteja kuhusu kesi yake na mahali ilipofikia.
4. Kupeana hundi gutu. Hili pia ni kosa la jinai.
5. Kukosa kuheshimu ahadi ya kitaaluma.
6. Kuchelewesha kesi (wakili kokosa kuchukua hatua za kuendeleza mashtaka ama kuhakikisha kesi inamalizika kwa wakati mwafaka)
7. Kukosa kujibu mawasiliano kutoka kwa mteja, wakili mwenzake ama Tume.
8. Kukosa kufuata maagizo ya mteja ama kuchukua hatua kinyume na maagizo ya mteja.
9. Kukosa kupeana stakabadhi ama hati za mteja haswa wakati mteja ametoa maagizo kutoka kwa wakili huyo. (Mteja amemuarifu wakili aache kumuwakilisha).
10. Kumlipisha mteja malipo ya ziada ama zaidi ya inavyotakikana.
11. Kulipisha chini ya malipo ambayo anatakikana kulipisha kulingana na mwongozo wa malipo wa mawakili.
12. Kukosa kwenda kortini wakati kesi iko na tarehe ya kusikizwa.
13. Kuhitilafiana/kutofautiana kwa maslahi ya wakili na mteja wake.
14. Kudai pesa kutoka kwa mtu ambaye si mteja wake.
15. Kufanya kazi bila cheti cha kuidhinishwa kutoka kwa chama cha mawakili wa Kenya kwa mwaka huo.

## Unapowakilishwa na wakili, zingatia yafuatayo:

1. Maagizo yote yameandikwa chini.
2. Umekubaliana na wakili kuhusu kiwango cha ama viwango vya malipo na jinsi ya kulipa na uhakikishe kuwa makubalino hayo yako katika maandishi.
3. Umefanya mawasiliano yote kwa maandishi.
4. Umepewa na kuhifadhi nakala za hati zote pamoja na mawasiliano baina yako na wakili.
5. Umeangalia hali ya kikazi ya wakili. Hii inaamanisha kuwa umeangalia na kuhakikisha kuwa wakili ako na idhini ya kufanya kazi, kwa kuangalia katika tovuti ya chama cha mawakili wa Kenya - (https://online.lsk.or.ke/)
6. Umepewa na kuhifadhi risiti zote za malipo.
7. Umekubaliana na wakili wigo wa ushiriki ama upeo wa kazi na makubaliano hayo yako katika maandishi.

## Malalamishi ambayo hayashughulikiwi na Tume:

1. Kesi zinazohusiana na uzembe wa wakili katika kazi yake.
2. Malalamishi dhidi ya maafisa wa mahakama na mawakili wa serikali.

## Mchakato wa Nidhamu katika Tume

